



Wito wa Kutuma Maombi juu ya Uwekezaji kupitia Programu ya Uwezeshaji Vijana na Wanawake Kiuchumi (*Youth and Women Economic Empowerment, YWEE*) Mkoani Kigoma

Maelezo kuhusu UNCDF

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Uwekezaji (UNCDF) ni shirika linalojikita katika uwekezaji maalumu kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi katika nchi 48 zenye maendeleo duni ulimwenguni. Kwa mamlaka na sheria zake za mitaji, UNCDF hutoaushauri juu ya namna ya kutengeneza maandiko ya kifedha ambayo ni kiungo muhimu katika kufungulia rasilimali za umma na binafsi, hasa katika ngazi ya chini katika jamii, ili kupunguza umaskini na kuyapa nguvu maendeleo ya kiuchumi ya eneo husika. Nchini Tanzania, UNCDF inasaidia miradi iliyobuniwa ili kufungulia upatikanaji wa mitaji kutoka soko la ndani na sekta binafsi ili kuwekeza katika miradi ya miundombinu midogo na ya kiwango cha kati, ambapo mitaji hii inahitajika ili kuongeza chachu ya maendeleo ya kiuchumi katika eneo husika na kuleta maendeleo kwa kushirikiana na sekta binafsi. Kwa kuimarisha namna mitaji ya kifedha inavyoweza kutumika katika ngazi ya mahalia, UNCDF inakuwa imechangia katika Lengo Namba 1 la Maendeleo Endelevu (Kupunguza Umaskini), la 5 (Usawa wa Jinsia), la 7 (Nishati Mbadala kwa Gharama Nafuu), la 9 (Viwanda, Ubunifu na Miundombinu) na la 17 (Ushirikiano wenye Malengo) kuhusu namna bora ya utekelezaji kwa kubaini maeneo mahitaji ya soko ambako kiubunifu na maandiko ya kifedha yanaweza kutumika ili kuleta matokeo yenye kuzaa matunda katika kusaidia kufikia malengo tarajiwa na kuleta usawa katika upatikanaji wa huduma.

Kuhusu Programu

UNCDF ni sehemu ya Programu ya Uwezeshaji Vijana na Wanawake Kiuchumi (YWEE) mkoani Kigoma, ambayo ni jitihada ya pamoja ya mahalia ya utayarishaji mipango na utekelezaji kupitia Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (2016 – 2021) kwa ajili ya Tanzania (UNDAP II). Programu hii inatekelezwa na UNCDF kwa kushirikiana na mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa ya UNDP, UNWomen, ILO, UNHCR, na ITC.

Wito wa Kutuma Maombi ya Uwekezaji

Kupitia wito huu, UNCDF inatoa mwaliko na kukaribisha maombi ya miradi ya uwekezaji inayoweza kutekelezwa kibiashara katika maeneo haya yanayolengwa:

- Uwezeshaji wanawake kiuchumi
 - *Miradi ya uwekezaji inayomilikiwa au kuendeshwa na wanawake au miradi ambayo wanawake ndiyo wanufaikaji wakubwa, kwa mfano, miradi midogo na ya kiwango cha kati ya miundombinu katika usindikaji mazao ya kilimo, uzalishaji wa viwanda na biashara, kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na nishati mbadala, na utoaji huduma za umma.*
- Uwezeshaji Vijana Kiuchumi na Ujasiriamali
 - *Miradi ya uwekezaji inayosimamiwa, kumilikiwa au kuendeshwa na vijana (vijana wake kwa waume wenye umri wa miaka kati ya 15-34) ambapo miradi hiyo inatoa ufumbuzi kwa changamoto zinazowakabili kama vile utengenezaji nafasi za ajira na kazi, kuwasaidia vijana kuingiza kipato, stadi za ufundi wa kibiashara, ubunifu, na ujasiriamali.*

Miradi ambayo manufaa yake kwa ujumla yanalenga kuwawezesha vijana na wanawake ikiwemo:

- Uzalishaji viwandani na usindikaji mazao ya kilimo
 - *Viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo, maghala ya kuhifadhia mazao ya kilimo na miradi mingine inayoongeza thamani katika shughuli za kilimo.*
- Miundombinu ya utoaji huduma kwa jamii kibiashara kuifanya iwe endelevu
 - *Kama vile: vituo vya mabasi, masoko na maeneo ya kuhifadhia bidhaa, miundombinu ya maji na miradi ya kusimamia taka.*
- Biashara
 - *Biashara ndogondogo na za kiwango cha kati ambazo zinawezesha muunganiko wa biashara na masoko katika mkoa wa Kigoma; na kati ya mkoa na chi za jirani kama vile DRC na Burundi.*
- Kujinusuru dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi na nishati mbadala
 - *Miradi inayoimarisha njia za kujipatia riziki kwa wanawake na kaya kwa ujumla. Hii ni pamoja na miradi ya miundombinu ya nishati mbadala kama vile uzalishaji umeme nje ya gridi ya taifa, malambo na mabwawa ya maji ya kilimo yanayoweza kusaidia kilimo cha umwagiliaji na cha kibiashara.*
- Maendeleo ya Kiuchumi ya Mahalia
 - *Biashara zinazotoa fursa kwa serikali za mitaa, sekta binafsi na jamii husika kushirikiana katika kuendeleza uchumi wa mahalia kwa kuimarisha uwezo wa kushindana, kuongeza ukuaji endelevu na kuhakikisha kuwa ukuaji huo ni jumuishi.*

Kile ambacho UNCDF inakusudia kukifanya kupitia YWEE

- Msaada wa kuandaa mradi
 - Inatoa msaada wa kiufundi katika kuandaa mradi na maandiko ya kifedha (kwa mfano, utunzaji bora wa kumbukumbu za mradi, tathmini na muundo wa kifedha wa mradi).
 - Kuandaa nyaraka za mradi wa uwekezaji kwa kuzingatia muundo unaokubalika katika taasisi za kifedha yakiwemo mabenki ya kibiashara na kwa wawekezaji.
- Kuwaunganisha wenye miradi na taasisi za fedha na wawekezaji
 - Kuwasaidia wenye miradi kupata fedha kutoka katika taasisi za kibiashara na za maendeleo (kwa mfano, kubaini wawekezaji sahihi kwa kutazama sekta husika, kutoa tathmini ya kiasi cha fedha na aina ya mtaji unaohitajika) na kusaidia kwenye mazungumzo a mapatano kuhusu masharti ya ukopaji.
 - Kwa miradi itakayopitishwa, UNCDF inaweza kutoa kianzio cha mtaji (mkopo wenye masharti nafuu au msaada wa fedha zinazoweza kurejeshwa) kulingana na mahitaji maalumu ya mradi husika na vigezo vya uwekezaji.
 - Kutoa msaada unaowezesha kukopesheka na msaada wa dhamana, kama sehemu ya dhamana ya mkopo kwa miradi itakayopitishwa ambayo inakidhi viwango vya kukopa kutoka katika taasisi za fedha za nchini.

Masharti ya kushiriki

Maombi ya miradi hayana budi kukidhi sifa zifuatazo:

- **Eneo la Kijiografia:** Wenye miradi ambayo inawalenga na kuwanufaisha vijana na wanawake kote katika Mkoa wa Kigoma wanahimizwa kutuma maombi. Upendeleo wa pekee utatolewa kwa miradi kutoka katika wilaya za **Kasulu**, **Kibondo** na **Kakonko**.
- **Maeneo ya mkazo wa mradi:** Ni muhimu miradi ya uwekezaji kuwa ni ile inayolenga maeneo ya: uwezesaji vijana na wanawake kiuchumi, usindikaji mazao ya kilimo na kuongeza thamani, miundombinu ya utoaji huduma kwa umma, biashara, kujinusu dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi na nishati mbadala.
- **Uwezekano wa kuendeshwa kibiashara:** Mapendekezo ya uwekezaji yatapaswa kuonyesha kuwa mradi utaingiza mapato, kupata faida na kuwa endelevu. Maombi ni lazima yaambatanishwe na maelezo ya kina ya gharama na mtiririko wa mapato na gharama za uendeshaji kuhusiana na mradi.
- **Matokeo chanya katika maendeleo:** Ni lazima mapendekezo yaonyeshe namna ambavyo mradi utaleta manufaa kwa jamii inayohusika, kama vile, kutengeneza nafasi za kazi, kuingiza kipato, uwezesaji wa makundi ya watu waliokosa fursa (wakiwemo wanawake, vijana na jamii za vijijini), upatikanaji wa biashara na masoko kwa ajili ya mazao ya kilimo.
- **Hali ya mradi kwa sasa:** Shughuli za kuandaa mradi ni lazima ziwe zimepitia hatua zote za awali za kupima uwezekano wa utekelezaji baada ya wazo la awali, yaani, maombi ni lazima yawe na mpango wa kibiashara na hatua zote za mwanzo za usajili zinazohitajika ni lazima ziwe zimeshapitiwa (kama vile, leseni, vibali, umiliki wa nyaraka n.k.). hivyo, kipaumbele kitatolewa kwa miradi iliyo tayari kuanza ambayo inalenga kupanua wigo wa uzalishaji.

- **Umiliki:** Mradi wa uwekezaji ni lazima uwe unaendeshwa na ama taasisi ya umma au sekta binafsi inayofanya kazi mkoani Kigoma, Tanzania.
- **Ukubwa wa mradi:** Wito huu unalenga miradi yenye ukubwa wa gharama za uwekezaji kati ya Dola za Marekani 50,000 na milioni 20.
- **Menejimenti:** Maombi ni lazima yaonyeshe kwamba mradi una timu ya menejimenti yenye stadi muhimu za kiufundi na kiutawala kumudu uendeshaji wa mradi.
- **Kuzingatia sheria:** Kukidhi matakwa ya sheria na kanuni za Tanzania na [Viwango vya Utendaji vya Kimazingira na Kijamii vya UNDCF/UNDP](#) ikiwemo haki za binadamu ni suala la lazima.

Vigezo vya Kuchaguliwa

Miradi yenye sifa itachaguliwa kwa ajili ya hatua nyingine zitazakofuata kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

- **Uwezekano wa kuendeshwa kibiashara:** Mapendekezo yanayoonyesha uwezekano wa kuingiza mapato na kutengeneza faida yatapewa kipaumbele.
- **Kuleta mabadiliko chanya ya kimaendeleo:** Kipaumbele kitatolewa kwa mapendekezo yanayoonyesha manufaa makubwa ya kimaendeleo ambayo jamii zinazohusika zitapata, kama vile, utengenezaji wa ajira, kuongeza mapato, kuwezesha makundi ya watu waliozikosa fursa wakiwemo wanawake, vijana na jamii za vijijini, kupatikana kwa biashara na masoko kwa ajili ya mazao ya kilimo, n.k.

Taarifa za Ziada

Kwa waombaji ambao watapita mchujo wa awali watapaswa kuwasilisha nyaraka zinazohusiana na mradi wao ndani ya majuma 2.

Kabla ya Kutuma Maombi Yako

UNCDF itatoa warsha ya nusu siku mnamo Jumatano, tarehe 13 Septemba, 2017 huko Ujiji, Kigoma ili kuwapa mwongozo waombaji kuhusu namna ya kuandaa maandiko na kutuma maombi. Lengo la mafunzo haya ni kuwapa waombaji fursa ya kuuliza maswali ili UNCDF itoe mwongozo kuhusu namna ya kuandaa maombi na kuongeza uwezekano wa kupata sifa zinazotakiwa na vigezo vya kuchaguliwa.

Ikiwa unataka kushiriki, tafadhali andika barua pepe kwenda local.finance@uncdf.org ukionyesha “YWEE Pre-submission workshop” kwenye kichwa cha habari cha barua pepe yako. Utaruhusiwa tu kushiriki katika warsha hiyo baada ya kupokea barua pepe kutoka UNCDF inayothibitisha kwamba tayari umesajiliwa kuhudhuria warsha hiyo. Muda na mahali pa warsha patatangazwa kadiri siku zinavyosogea kwa wale ambao watatuma maombi kupitia barua pepe.

Kumbuka kwamba si lazima kushiriki katika warsha hiyo iliuweze kutuma maombi ya mradi wako. Warsha hii ni kwa hisani tu inayotolewa na UNCDF.

Maelekezo ya namna ya kutuma mapendekezo

Ni yale maombi tu yaliyokamilika kwa mujibu wa maelekezo ndiyo yatakayopitiwa. Maombi yaliyokamilika yatahusisha fomu mbili tofauti za utumaji ambapo mwombaji ni lazima ajaze kikamilifu maeneo yote:

1. Fomu ya Wito wa Kutuma Mapendekezo (programu ya Word) ambayo inaweza kupatikana kwenye ukurasa huu
2. www.uncdf.org/download/file/127/4099/2a-submissionkipyweeformworddocx
3. Fomu ya Wito wa Kutuma Mapendekezo (**programu ya Excel**) ambayo inaweza kupatikana kwenye ukurasa huu
www.uncdf.org/download/file/127/4100/2b-submissionkipyweeformexcelxlsx

Nyaraka nyingine za ziada ni lazima zitumwe tofauti.

Fomu hizo mbili za kutuma maombi (kwenye programu za Word na Excel) **ni lazima ziwasilishwe** katika muundo wake wa asili (kwenye programu za Word na Excel) pamoja na nyaraka nyingine za nyongeza kwenda kwa anwani ya: local.finance@uncdf.org. Zingatia kwamba ni ombi moja tu kwa taasisi na kwa kila pendekezo litapokelewa.

Lugha itakayotumika katika mapendekezo: Mapendekezo ni lazima yaandaliwe kwa lugha ya **Kiingereza**.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi: Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya mapendekezo ya uwekezaji ni Septemba 25, 2017.

Tafadhali zingatia: Waombaji ambao hawatatumia hizo fomu katika kuwasilisha maombi yao ndani ya muda uliopangwa, basi maombi hayo hayatafanyiwa kazi. Waombaji watakaofuzu tu hatua ya awali ndio watakaopewa majibu ya maombi yao ndani ya majuma 3 baada ya tarehe ya mwisho ya maombi. Hivyo basi, wale waombaji ambao hawatapata majibu ndani ya muda huo wajue kuwa maombi yao hayakufanikiwa.